# AJENDA YA UTAFITI WA PAMOJA WA AFRIKA

## YA KUKOMESHA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

### MUHTASARI

NOVEMBA 2023

SVRI sexual violence research initiative

UN WOMEN

# Muhtasari

Ajenda ya Utafiti wa Pamoja wa Afrika (ASRA) ya kukomesha Unyanyasaji wa Kijinsia (UWAKI) ni msururu wa mapendekezo ya Vipaumbele vya tafiti ambavyo vimetambuliwa mchakato madhubuti, wa kina na jumuishi unaozingatia maoni na sauti za walengwa wa utafiti. Ni mbinu ya kipekee na imara kwenye kushughulikia azma ya ushirikiano na nguvu ya pamoja katika kukomesha UWAKI.

ASRA inafuatia kuundwa, kwa Ajenda ya Utafiti wa Pamoja wa Ulimwenguni (GSRA) mwaka wa 2021, ushirikiano kati ya Mpango wa Utafiti wa Unyanyasaji wa Kijinsia (UWAKI) na Taasisi ya Usawa (EQI), kwa msaada wa washirika wa ufadhili na nyanjani. GSRA iliwasilisha matokeo ya midahalo na mijadala yenye ushahidi wa miaka miwili, ambayo ilitokana na hekima ya watu wengi kuweka vipaumbele vya utafiti kwa miaka mitano ijayo kwa ajili ya utafiti wa haki, madhubuti na unaofaa kuhusu unyanyasaji dhidi ya wanawake (VAW) kwenye nchi za kipato cha chini na kati. Kwa mara ya kwanza, sauti za watendaji, wanaharakati, na manusura zilijumuishwa pamoja na zile za wasomi na wataalamu wengine.

Ili kutambua vipaumbele vya utafiti, na kuhakikisha mchakato huo ulikuwa wa haki na uwazi, mbinu iitwayo Child Health and Nutrition Research Initiative (CHNRI) ilitumika, ikizingatia maoni ya wadau wengi, na siyo ya wataalam pekee, hivyo maoni yote yanashughulikiwa kwa usawa bila sauti nyingine kuwa na ushawishi zaidi kuliko nyingine. Hilo linafanywa kwa 'Ukusanyaji taarifa moja kwa moja kutoka kwa raia' ili kupata maoni mengi kuhusu suala fulani, kuliko mtazamo wa 'kitaalam' wa mtu mmoja.

GSRA ilionyesha hitaji la utafiti kuhusu mbinu za kuzuia UWAKI na ufanikishaji wa uwekezaji wa programu na sera. Kwa kutambua miktadha tofauti ambapo unyanyasaji unaochochewa na ukosefu wa usawa wa kijinsia unajidhihirisha katika bara zima la Afrika, ilionekana wazi ni muhimu kuanzisha GSRA ya ndani ili kubainisha maeneo ya utafiti ya kipaumbele kikanda. Wanawake na wasichana balehe katika Afrika ya Kati, Mashariki, Magharibi na Kusini walikabiliwa na viwango vikubwa vya Ukatili wa kimwili na kingono kwenye mwaka uliopita, ambavyo ni vya juu zaidi kuliko makadirio ya kimataifa. Kwa sababu hii, kujenga ushahidi na uundaji wa maarifa kwa kanda hizi ndogo za Afrika ni muhimu kwa ajili ya maendeleo na uwajibikaji kwa wanawake na wasichana katika utofauti wao wote kupitia utoaji wa programu bora na zenye ufanisi mkubwa.

Kwa kujifunza kutoka kwenye mchakato wa GSRA, UN Women (kupitia Ofisi za Kanda za Afrika Mashariki na Kusini na Afrika Magharibi na Kati) na Mpango wa Utafiti wa Dhuluma za Kijinsia (SVRI) wameshirikiana na wadau wengine tangu Mei 2022 ili Kuunda kikundi cha vipaumbele vya pamoja vya utafiti wa kikanda kwa Afrika ili kuongoza, kuweka utaratibu na kuvutia fedha kwa ajili ya Kukusanya na kuweka ushahidi wa UWAKI.

Vikundi vitatu vilianzishwa ili kutawala na kuongoza ASRA:

1. KIKUNDI CHA USIMAMIZI: Wafanyakazi wakuu wanaofanya kazi na SVRI na Ofisi za Kanda za UN Women katika Afrika Mashariki na Kusini na Afrika Magharibi na Kati.
2. KIKUNDI CHA USHAURI: Kundi la wataalam 26 waliobobea katika kuzuia na kukabiliana na VAW/UWAKI, kwa kuzingatia kanda za Mashariki, Kati, Magharibi na Kusini mwa Afrika, lilitambuliwa na Kikundi cha Usimamizi. Kikundi cha Ushauri kilijumuisha watu kutoka kanda ndogo za Afrika wenye asili mbalimbali, ikiwa ni pamoja na utetezi, utafiti na taasisi za kitaaluma, mashirika ya kiraia, taasisi za uhisani na mfumo wa Umoja wa Mataifa.
3. KIKUNDI CHA KIKANDA CHA WATAALAMU: Kundi la takriban wataalam 400 wa kikanda kutoka Mashariki, Kati, Magharibi na Kusini mwa Afrika wanaofanya kazi ya kuzuia na kukabiliana na GBV, wakiwamo watafiti, watendaji, mashirika ya haki za wanawake na ufeministi, wanaharakati na mitandao, wafadhili, watunga sera na wengine.

Kwa kuongozwa na miundo hii, iliyojaa uanuwai na shauku ya nyanjani, ASRA ilitengeneza mchakato wa ushirikishi wa hatua saba na kimwingiliano, wenye fursa nyingi za maoni, ukaguzi na changamoto kutoka kwa wanakikundi tofauti wa utawala na ushauri. Hatua ya kwanza ilihusisha ukaguzi wa fasihi, ili kubaini mapungufu muhimu katika Nyanja ambayo yalitayarisha mchakato wa kuweka kipaumbele na kutambua vikoa vitano

Translation reviewed by Aisha Majengo

muhimu vya utafiti:

KIKOA CHA 1: UFAHAMU WA UWAKI
KIKOA CHA 2: HATUA ZA KUKABILI UWAKI
KIKOA CHA 3: HATUA ZA KUZUIA UWAKI
KIKOA CHA 4: MWITIKO WA UWAKI NA KIWANGO CHA UZUIAJI
KIKOA CHA 5: MBINU NA VIPIMO

Vikoa vilipobainishwa, maswali ya utafiti yalikusanywa kutumia mbinu ya awamu mbili ¬– utafiti wa kukusanya maswali mtandaoni ulioshirikiwa na Kikundi cha Usimamizi, Kikundi cha Ushauri na Kikundi cha Wataalamu wa Kikanda, na mahojiano ya watoa habari mtandaoni (KIIs) na mijadala ya vikundi lengwa (FGDs) pamoja na wataalam. Maswali 508 yaliunganishwa na kufanywa kipaumbele na Kikundi cha Usimamizi kupitia mchakato wa awamu mbili, na kupunguzwa hadi 49, takriban maswali kumi kwa kila kikoa. Kisha maswali yalisambazwa kwenye vikundi mbalimbali vya utawala kupitia uchunguzi wa mtandaoni, ambapo wahojiwa walitakiwa kuorodhesha maswali ya utafiti katika kila kikoa, na kwa jumla. Jumla ya wataalam 186 walituma majibu yao ya utafiti.

Maswali mawili makuu yaliyoorodheshwa katika kila kikoa ni:

## KIKOA CHA 1: UFAHAMU WA UWAKI

1. Je, ni hali na aina gani za UWAKI zinazoathiri hasa wanawake na wasichana wenye ulemavu, na wanawake na wasichana wanaoishi na VVU/UKIMWI, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, ndoa za utotoni, unyanyasaji wa kimuundo (k.m., kunyimwa huduma za afya, elimu na sheria) na unyanyasaji wa kiuzazi (k.m., kuzuia mimba kwa lazima au kufunga kizazi)?

2. Ni dhana zipi za kijamii na kijinsia, ikiwa ni pamoja na mila na desturi za uanaume, zina athari (hasi au chanya) kwenye Unyanyaji wa Kijsinia UWAKI

## KIKOA CHA 2: HATUA ZA KUKABILI UWAKI

1. Je, usaidizi wa UWAKI wa sekta mbalimbali (k.m., huduma za afya, sheria, elimu na uwezeshaji) unaweza kubadilika kulingana na miktadha tofauti ya mahitaji na sifa za waathiriwa/manusura, ikiwa ni pamoja na wale kutoka jamii zilizotengwa?

2. Je, tafsiri tofauti za 'haki' zinatuonesha nini kuhusu jinsi ya kuunda programu za haki kwa waathiriwa wa unyanyasaji?

## KIKOA CHA 3: HATUA ZA KUZUIA UWAKI

1. Ni hatua zipi zinazotumika kwa viongozi wa kidini na/au wa kimila, au miundo mingine ya kijamii yenye mfumo dume, ambayo imefanikiwa zaidi katika kuzuia UWAKI na kwa nini?

2. Ni hatua zipi za jamii za kiasili ambazo zimetengenezwa na kutumika kuzuia UWAKI, na zimefanikiwa kwa kiasi gani?

## KIKOA CHA 4: MWITIKO WA UWAKI NA KIWANGO CHA UZUIAJI

1. Ni hatua zipi za kuzuia UWAKI, zikijumuisha mabadiliko ya desturi za kijamii na mwitiko wa wanandoa, zinaweza/zinapaswa kuongezwa katika mazingira ya chini ya rasilimali na vijijini?

2. Je, ni jinsi gani miundombinu ya ngazi ya jamii na mashirika ya kijamii yanayosaidia kuzuia na kukabiliana na UWAKI inaweza kuimarishwa, kutaalamishwa na kuchukuliwa kwenye viwango kupitia mifumo ya serikali, hasa katika mazingira yenye rasilimali chache?

## KIKOA CHA 5: MBINU NA VIPIMO

1. Je, tunawezaje kuboresha mbinu za utafiti ili kuongeza usahihi wa data na kuripoti kuhusu UWAKI?

2. Je, ni vipi tunaweza kujumuisha uzalishaji maarifa Asilia na desturi katika uendeshaji wa utafiti wa kimaadili wa viwango vya juu kuhusu UWAKI?

Mchakato wa kupanga kipaumbele wa ASRA umefichua mafunzo muhimu kuhusu vipaumbele vya utafiti ili kuendeleza uwanja wa kuzuia na kukabiliana na UWAKI barani Afrika, na mbinu iliyotumika kutambua vipaumbele hivi.

Ingawa kulikuwa na tofauti fulani katika vipaumbele vya utafiti kulingana na sifa za wataalam, kwa ujumla, kulikuwa na makubaliano makubwa kwenye maswali matano ya juu kwa kila kikoa. Mchakato pia ulibainisha umuhimu wa kunyumbulika, wa kutilia maanani kuondoa ukoloni na kukuza mchakato jumuishi zaidi wa kufanya kipaumbele cha utafiti. Mbinu ya ASRA ilibidi iendane na maoni haya.

Mbinu mseto pia ni muhimu kwa kuweka kipaumbele. Michakato ya awali ya kuweka ajenda ya utafiti imekuwa mazoezi ya kiasi cha kulingana na wazo la 'Ukusanyaji taarifa moja kwa moja kutoka kwa wananchi kwenye maswali ya utafiti yaliyofanywa kipaumbele zaidi. Kwa kuongeza mbinu za ubora, mchakato jumuishi zaidi uliundwa ambao uliwezesha vikundi vidogo vya watu maalum, hasa vinavyokabiliana na aina zinazopingana za ubaguzi, kushiriki kikamilifu zaidi katika kuweka kipaumbele

Licha ya kuwa jumuishi na ya kidemokrasi, zoezi la kuweka vipaumbele linaweza pia kuwa la upendeleo. Mchakato na mbinu ya ASRA iliinua kwa makusudi sauti za wataalam mbalimbali wa UWAKI, wakiwamo wale wanaofanya kazi na makundi yaliyotengwa. Mbinu ya CHNRI inajaribu kupunguza upendeleo huo kupitia mbinu yake ya ukusanyaji taarifa moja kwa moja kutoka kwa wananchi; hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba upendeleo bado unaweza kutokea.

Kuna uwiano mzuri kati ya kupunguza upendeleo na kuongeza ushiriki. Hatua ya kuelekea katika zoezi jumuishi zaidi na shirikishi la kuweka vipaumbele vya utafiti inahitaji uwiano wa kurekebisha mbinu ili kuzingatia miundo ya kisiasa na mamlaka ambayo ni asili ya mazoezi ya kipaumbele ya jadi ya utafiti, wakati pia kuzingatia jinsi ya kuweka kiini cha kukusanya 'hekima ya watu wengi'. Kwa mfano, mbinu ya kawaida ya CHNRI hutumia tafiti kukusanya maswali ya utafiti na kupata alama za maswali haya, ambayo inachukulia kuwa wahojiwa wote watakuwa na ufikiaji na uelewa sawa wa kujihusisha katika tafiti hizo. Kwa kweli, kubuni swali la utafiti si kazi rahisi, na kwa wataalam wa UWAKI ambao hawana usuli wa utafiti, hii inaweza kuwa changamoto na kuwafanya wahusika kujiondoa kwenye mchakato.

Vipaumbele vya utafiti vinapaswa kutafsiriwa kulingana na ushahidi uliopo. Kwa kuzingatia uwepo wa shughuli kadhaa za tafiti za kuweka vipaumbele kuhusiana na UWAKI tangu mwaka 2015, ni muhimu kuhakikisha michakato inazingatia na kujifunza kutokana na matokeo ya shughuli za awali.

Kama uzoefu wa ASRA unavyoonyesha, kukamilisha shughuli ya kuweka kipaumbele kunaweza kuwa jambo gumu na la kutumia muda mwingi. Lakini mchakato wa kuweka kipaumbele ni muhimu kama mbinu, hasa haja ya kuhakikisha sauti mbalimbali zinajumuishwa. Hatimaye, ASRA itakuwa na ufanisi ikiwa tu matokeo yatatumika. Wafadhili wanapaswa kuongeza uwekezaji katika utafiti wa ubora wa hali ya juu na wa kimaadili unaowiana na ASRA; watafiti wanafaa kutumia ASRA kwenye ajenda zao za utafiti; watendaji wanapaswa kutumia ajenda kama mwongozo wa ushirikiano na watafiti kuhusu tathmini ya miitiko yao; na kama uwanja mmoja, ASRA inapaswa kutumika kama marejeleo ya kutetea ufadhili zaidi na bora kwa utafiti ambao unashughulikia mianya muhimu ya utafiti na maarifa katika uwanja huo.

UN Women in Africa na Mpango wa Utafiti wa Unyanyasaji wa Kijinsia (UWAKI) zimejitolea kuchangia ulimwengu ambao wanawake katika utofauti wao wote na watoto wanaweza kufurahia haki yao ya kuishi bila unyanyasaji. Kwa kutambua uwezo wa uzalishaji wa maarifa na hitaji la michakato ya utafiti iliyo sawa na jumuishi zaidi katika juhudi za kukomesha UWAKI, UN Women na SVRI zimeshirikiana kuwezesha Ajenda ya Utafiti wa Pamoja wa Afrika kwa ajili ya kukomesha UWAKI (ASRA).

Ajenda ya Utafiti wa Pamoja wa Afrika (ASRA) ya kukomesha unyanyasaji wa kijinsia (UWAKI) ni msururu wa mapendekezo ya Vipaumbele vya tafiti ambavyo vimetambuliwa kwa mchakato madhubuti, wa kina na jumuishi unaozingatia maoni na sauti za walengwa wa utafiti. Ni mbinu ya kipekee na imara kwenye kushughulikia azma ya ushirikiano na juhudi ya pamoja katika kukomesha UWAKI. ASRA inatokana na masomo ya Ajenda ya Utafiti wa Pamoja wa Ulimwenguni kuhusu Unyanyasaji dhidi ya Wanawake na imeundwa kupitia mchakato wa pamoja kwa kujifunza na kushauriana. Ni mchango kwenye mpango wa Generation Equality Action kuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia na hutoa maarifa katika maswali muhimu ya utafiti yaliyotambuliwa kama vipaumbele vya kukomesha UWAKI na wataalam mbalimbali wanaoishi na kufanya kazi katika Afrika ya Kati, Mashariki, Kusini na Afrika Magharibi.

SVRI sexual violence research initiative

UN WOMEN